**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

# MWONGOZO WA UTOAJI WA ELIMU YA KUJITEGEMEA KATIKA SHULE ZA MSINGI NA SEKONDARI TANZANIA BARA

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

Toleo la Kwanza 2022

ISBN: 978_9987_09_518_6

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia
Mtaa wa Afya – Mtumba
P. O. Box 10
40479 Dodoma
Tel: +255 26 296 3533
Email: info@moe.go.tz

Haki zote zimehifadhiwa.  Hairuhusiwi kunakili, kutafsiri, kurudufu, kupiga chapa wala kutoa andiko hili kwa namna yoyote ile bila idhini ya Kamishna wa Elimu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

**Mwongozo huu umetayarishwa na: Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia**
**Januari, 2022**

# YALIYOMO


**DIBAJI** ........................................................................................................ vi

1.0 Utangulizi.................................................................................................. 1

1.1 Usuli .......................................................................................................... 1

2.0 Lengo la Mwongozo wa Utoaji wa Elimu ya Kujitegemea katika Utekelezaji wa Miradi ya Uzalishaji mali............................................ 2

2.1 Dhana ya Elimu ya Kujitegemea katika Miradi ya Uzalishaji Mali.... 2

2.2 Namna Elimu ya Kujitegemea itakavyotolewa shuleni....................... 3

2.3 Umuhimu wa Utoaji wa Elimu ya Kujitegemea katika Miradi ya Uzalishaji Mali Shuleni.............................................................................. 3

2.4 Matokeo ya Utoaji wa Elimu ya Kujitegemea katika Miradi ya Uzalishaji Mali........................................................................................... 4

3.0 Namna ya Kuendeshaji wa Miradi ya Uzalishaji Mali ....................... 4

4.0 Hatua za Uanzishaji na Utekelezaji Miradi ya Uzalishaji Mali........... 5

5.0 Usimamizi wa Miradi ya Uzalishaji Mali ........................................... 5

6.0 Majukumu ya Wadau Mbalimbali ........................................................ 6

6.1 Kamati/Bodi ya Shule ............................................................................ 6

6.2 Mwalimu Mkuu/Mkuu wa Shule ......................................................... 6

6.3 Kamati ya Elimu ya Kujitegemea .......................................................... 7

6.4 Afisa Elimu Kata, Halmashauri na Mkoa ............................................ 8

6.5 Maofisa Maendeleo ya Jamii ................................................................ 8

6.6 Mratibu wa Elimu ya Kujitegemea ....................................................... 8

6.7 Kiongozi wa Wanafunzi wa Elimu ya Kujitegemea .......................... 8

6.8 Mhasibu wa Shule.................................................................................. 9

7.0 Matumizi ya Mapato yanayotokana na Miradi ya KuzalishaMali....... 9

8.0 Uuzaji wa Mazao au Vifaa/Bidhaa ....................................................... 9

9.0 Motisha kwa Wanafunzi na Wafanyakazi ............................................ 9

10.0 Ukaguzi wa Fedha za Miradi ya Sshule .............................................. 10

11.0 Taarifa ya Uzalishaji Mali .................................................................... 10
12.0 Hitimisho.................................................................................................. 10
**Rejea**............................................................................................................ 11

# DIBAJI

Serikali imeazimia kuboresha elimu nchini kwa kuweka mazingira bora, salama na kuhakikisha kuwa huduma muhimu zikiwemo miundombinu, vifaa, chakula bora, mawasiliano, maji salama na afya zinapatikana shuleni ili kuwezesha ufundishaji na ujifunzaji wenye ufanisi. Azma hiyo imefafanuliwa katika Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 na Mpango wa Maendeleo ya Elimu wa Miaka Mitano (ESDP 2016/17-2020/21). Msingi wa elimu na mafunzo umejikita katika kumjengea Mtanzania misingi bora ya malezi, maadili, ujuzi (maarifa na stadi), umahiri na kumwezesha kujitegemea. Malengo hayo yatafikiwa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa elimu wakiwemo wanafunzi, walimu na jamii kwa ujumla.

Sera ya Elimu na Mafunzo iliyopo imeeleza umuhimu wa kuwa na miradi ya uzalishaji mali katika shule za msingi na sekondari. Shule zinapaswa kubuni, kuanzisha na kutekeleza miradi mbalimbali katika maeneo yao kwa kuzingatia mazingira ya shule husika. Ni muhimu kuzingatia kwamba falsafa ya Elimu ya Kujitegemea (EK) itaendelea kuongoza utoaji wa elimu na mafunzo kwa kuzingatia mabadiliko yanayotokea katika jamii, kiuchumi, kijamii, kiutamaduni, kisiasa, kisayansi na kiteknolojia.
Ili kuboresha ushiriki wa jamii, Serikali imetoa Kiongozi cha Mwalimu Mkuu cha Uboreshaji wa Elimu katika Shule za Msingi mwaka 2013 kinachoelekeza kuanzisha, kusimamia na kufanya tathimini ya miradi ya shule ikiwa ni pamoja na kufuatilia mapato na matumizi yatokanayo na miradi iliyoanzishwa shuleni. Kwa kuzingatia maelekezo hayo, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inatoa Mwongozo huu wa Utoaji wa Elimu ya Kujitegemea kupitia Miradi ya Uzalishaji Mali shuleni.

Mwongozo huu utasaidia Afisa Elimu Kata, Mwalimu Mkuu/ Mkuu wa Shule, Kamati/ Bodi za Shule, Mwanafunzi na Jamii kwa ujumla katika utekelezaji wa falsafa ya Elimu ya Kujitegemea. Ni matarajio ya Serikali kuwa mwongozo huu utakuwa nyenzo muhimu ya kuwajengea misingi bora ya malezi, maadili, ujuzi, maarifa, Stadi, umahiri na kumwezesha mwanafunzi kujitegemea.

Matokeo ni kukuza uzalendo katika fikra zenye mwelekeo chanya kuhusu matumizi ya akili ili kubaini fursa mbalimbali zilizo kwenye mazingira yanayowazunguka na kutumia rasilimali zilizopo ili kuleta maendeleo binafsi, jamii na Taifa kwa ujumla.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
Kamishna wa Elimu
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

## 1.0 Utangulizi

Mwongozo wa Utoaji wa Elimu ya Kujitegemea kupitia Miradi ya Uzalishaji Mali katika Shule za Msingi na Sekondari unatoa maelezo yanayobainisha namna shule zinavyoweza kuanzisha na kusimamia utekelezaji wa miradi ya uzalishaji mali kwa ufanisi na tija. Kupitia Mwongozo huu, shule zina fursa ya kuanzisha miradi kwa kuzingatia mahitaji na mazingira ya shule husika. Mwongozo huu utatumika katika shule za Msingi na Sekondari kuanzia Darasa la Kwanza hadi Kidato cha Sita.

## 1.1 Usuli

Kwa kipindi cha takribani miongo mitatu iliyopita shule za msingi, sekondari na vyuo vya kati vilitumia miradi kama sehemu ya kuoanisha mafunzo ya nadharia na vitendo. Uzoefu wa utekelezaji wa programu za uzalishaji mali umeonesha kuwa na mafanikio makubwa katika kuziwezesha shule kujipatia baadhi ya mahitaji na kujenga dhana ya uwajibikaji, kupenda kazi na uzalendo kwa wanafunzi. Inafahamika kuwa, zipo baadhi ya shule ambazo zina miradi ya uzalishaji mali ambayo inaendeshwa na kusimamiwa kwa ufanisi mkubwa. Shule hizo zinaweza kutumika kama sehemu ya kujifunza kwa shule ambazo hazina miradi ya namna hiyo.

Hata hivyo, miradi mingi ya uzalishaji mali shuleni imekuwa duni na dhaifu na baadhi kufutika kutokana na kutokuwepo kwa elimu ya kujitegemea, usimamizi imara wa miradi na kukosekana kwa uwazi wa mapato na matumizi. Kwa kuzingatia changamoto mbalimbali zilizopo katika uanzishaji, usimamizi na uendeshaji wa miradi ya uzalishaji mali, imeonekana kuwa ni muhimu kuwepo kwa mwongozo unaotoa maelekezo ya namna ya utoaji wa elimu ya uanzishaji, usimamizi na utekelezaji wa miradi ya uzalishaji mali miongoni mwa wanafunzi, walimu na watumishi wasio walimu kwa nadharia na vitendo. Aidha, wapo walimu wenye uzoefu na maarifa makubwa ya kuendesha miradi ya namna hii, maofisa wenye ujuzi wa kusimamia miradi ya uzalishaji mali katika jamii ngazi ya kijiji/mtaa, Kata na Halmashauri. Hivyo, endapo watabainishwa na kushirikishwa watatumia vizuri uzoefu wao kutaongeza tija katika miradi hii hususan katika utoaji wa Elimu ya Kujitegemea ikiwemo elimu ya uzalishaji mali.

## 2.0 Lengo la Mwongozo wa Utoaji wa Elimu ya Kujitegemea katika Utekelezaji wa Miradi ya Uzalishaji Mali

Mwongozo umeandaliwa ili kukidhi malengo yafuatayo:

a) Kuiwezesha shule kuweka utaratibu wa kutoa Elimu ya Kujitegemea ili kuwajengea uwezo wa kubuni, kuanzisha na kusimamia miradi ya uzalishajimali shuleni;

b) Kuimarisha miradi anuai ya kujitegemea ambayo imekuwa ikitekelezwa na shule kama sehemu ya kutafsiri kwa vitendo falsafa ya Elimu ya Kujitegemea;

c) Mwongozo utaziwezesha shule kuanzisha na kusimamia Utoaji wa Elimu ya kujitegemea katika kutekeleza miradi ya uzalishaji mali kwa ufanisi. Kila shule ni sharti iwe na mradi au miradi ya uzalishaji mali kwa kuzingatia Jiografia na fursa za eneo husika;

d) Kuwezesha shule kubuni na kuibua aina ya miradi ya kujitegemea kwa kusaidiana na wataalamu waliopo katika shule na jamii iliyopo karibu na shule katika ngazi ya Kijiji/ Mtaa, Kata na Halmashauri wanaoweza kutoa utaalamu na elimu juu ya uanzishaji na usimamizi wa miradi mbalimbali;

e) Kuainisha majukumu na wajibu wa wadau mbalimbali katika kutekeleza utoaji wa Elimu ya Kujitegemea katika uanzishaji na usimamizi wa miradi kwa kuzingatia jiografia na fursa za eneo husika; na

f) Mwongozo unabainisha muda kwa kila shule wa kufanya shughuli za Elimu ya kujitegemea zikiwemo za uzalishaji mali bila kuathiri muda wa ufundishaji na ujifunzaji darasani unaozingatia uwezo na mahitaji ya wadau shuleni.

## 2.1 Dhana ya Elimu ya Kujitegemea katika Miradi ya Uzalishaji Mali

Elimu ya kujitegemea ni maarifa ambayo mtu hujengewa misingi bora ya malezi, maadili, ujuzi (maarifa na stadi), umahiri na kumwezesha kujitegemea. Moja ya misingi ya kuimarisha na kuendeleza dhana ya kujitegemea ni kutoa elimu ya uzalishaji mali shuleni kwa vitendo. Shughuli yoyote ambayo inaipatia shule kipato halali inaweza kuitwa mradi wa uzalishaji mali. Shughuli hizo ni kama vile kilimo cha mboga mboga, nafaka, jamii ya mikunde na mbegu za mafuta; ufugaji wa kuku, mbuzi, kondoo, sungura, ng’ombe, samaki na nyuki;

na biashara kama duka, chakula, ushonaji, mashine za kukoboa na kusaga nafaka na kukamua mbegu za mafuta, na mashine za kuchomelea na kukata vyuma.

## 2.2 Namna Elimu ya Kujitegemea itakavyotolewa shuleni

Elimu ya kujitegemea inaweza kutolewa kupitia:

i) Vyama vya masomo kuhusu namna ya kuanzisha na kusimamia miradi;

ii) Kupitia "project" mbalimbali zinazoanzishwa shuleni;

iii) Elimu mtambuka kupitia masomo ya Uraia, Stadi za maisha Kilimo, Biashara na Uchumi (Account, Book keeping, Commerce, Economics) na Jiografia;

iv) Kutumia walimu wenye uzoefu, maarifa, ujuzi, na Stadi za maisha kuhusu uendeshaji wa miradi;

v) Kutumia wataalamu waliopo katika ofisi za watendaji wa kijiji / Mtaa/Kata kutoa eilmu namna ya uandaaji na uendeshaji wa miradi (Afisa maendeleo, Afisa kilimo, Afisa mipango na Uchumi);

vi) Kupitia midahalo, mijadala na vikao vya wafanyakazi katika maeneo yao, madarasani, na mabwenini; na Ushirikishaji wa wanajamii walio karibu na shule na taasisi mbalimbali zinazochangia katika maendeleo ya elimu na uelimishaji rika.

## 2.3 Umuhimu wa Elimu ya Kujitegemea katika Miradi ya Uzalishaji Mali Shuleni

Miradi ya Uzalishaji mali Shuleni ina lengo la kuwajengea uwezo na uzoefu wa kuzalisha mali na kuendeleza uchumi ndani ya shule na hata baada ya kumaliza shule. Kupitia miradi, wanafunzi, watumishi wasio walimu na walimu wanapata maarifa ya namna ya kubuni na kutumia fursa katika kuanzisha miradi itakayowaletea maendeleo yao binafsi, jamii na taifa kwa ujumla. Pamoja na lengo hilo, miradi inayotekelezwa inapaswa kujiendesha na kuchangia katika maendeleo ya Shule. Miradi hii itasaidia katika mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja na:

i) Kuwajengea wanafunzi stadi za uzalishaji mali kwa vitendo na Ubunifu;

ii) Kuwawezesha wanafunzi kuoanisha/kutafsiri nadharia kwa vitendo;

iii) Kuzipatia shule kipato kwa ajili ya kuendesha shughuli mbalimbali;

iv) Kujenga uzalendo na umoja shuleni kupitia kazi;

v) kusaidia kutekeleza mipango ya shule;

vi) Kuiwezesha shule kutoa huduma muhimu kama vile chakula, kulipia ankara za maji na umeme, motisha kwa walimu na wanafunzi; na

vii) Kusaidia katika kuboresha miundombinu na samani za shule.

## 2.4 Matokeo ya Elimu ya Kujitegemea katika Miradi ya Uzalishaji Mali Shukleni

Matarajio ya utoaji wa Elimu ya Kujitegemea katika Miradi ya Uzalishaji mali Shuleni ni kuwa na mtanzania aliye elimika, mwenye ujuzi, maarifa, stadi, umahiri na malezi bora ili kumwezesha kujitegemea na kuchangia katika maendeleo ya nchi kiuchumi. na anayeweza kujitegemea katika misingi bora ya malezi, maadili, ujuzi (maarifa na stadi), umahiri, uzalendo na kumwezesha kujitegemea. Elimu ya kujitegemea inasaidia Taifa kuwa na wananchi walioelimika watakaoweza kushiriki kikamilifu katika ujenzi wa taifa kwa vitendo. Pia, inaisidia shule kupata kipato kwa ajili ya kuendesha katika shughuli mbalimbali.

## 3.0 Namna ya Kuendeshaji wa Miradi ya Uzalishaji Mali

Ili kuwezesha uendeshaji wa miradi ya uzalishaji mali kufanyika kwa ufanisi na ujifunzaji;

a) Kila shule itenge muda ambao hautaathiri muda wa ufundishaji darasani kwa ajili ya kufanya kazi za uzalishaji mali baada ya muda wa masomo;

b) Ratiba ya vipindi vya uzalishaji mali ibainishwe katika ratiba ya kila siku ya utekelezaji wa shughuli za shule nje ya darasa; na

c) Katika kuanzisha au kuendeleza miradi ya uzalishaji mali ni vema kupata uzoefu kutoka kwa wadau, taasisi zilizofanikiwa au zenye utaalamu katika uendeshaji wa miradi.

## 4.0 Hatua za Uanzishaji na Utekelezaji Miradi ya Uzalishaji Mali Katika kuanzisha Miradi mbalimbali ya uzalishaji mali ni muhimu kuzingatia yafuatayo:

a) Kamati/Bodi ya Shule iandae Vikao vya Walimu na Wanafunzi kuhusu uanzishaji wa miradi ya uzalishaji mali ya shule kwa kuangalia changamoto zilizoainishwa kwenye Mpango wa Jumla wa Maendeleo ya Shule;

b) Kamati/Bodi ya Shule, Walimu na wanafunzi wabainishe fursa na aina ya miradi inayoweza kutekelezwa kutokana na fursa zilizopo.

c) Kamati ya Uzalishaji mali iandae andiko la mradi na kupitishwa na Kamati/ Bodi ya Shule kwa ajili ya kuridhiwa; na

d) Wanajumuiya wa shule washirikishwe katika kutekeleza mradi uliokubaliwa.

## 5.0 Usimamizi wa Miradi ya Uzalishaji Mali

Ili kuwa na usimamizi bora wa miradi, uongozi wa shule utahakikisha yafuatayo yanatekelezwa:

a) Kuunda kamati ya elimu ya kujitegemea (EK) itakayokuwa na jukumu la kusimamia utekelezaji wa miradi ya shule;

b) Uongozi wa shule utaweka utaratibu wa usimamizi wa mradi na kuunda Kamati ya usimamizi wa mradi;

c) Kamati ya Elimu ya Kujitegemea itafanya kazi chini ya usimamaizi wa kiongozi;

d) Kamati ya Usimamizi wa mradi itakuwa na jukumu la kusimamia utekelezaji wa mradi kila siku chini ya usimamizi wa Kamati/Bodi ya Shule; na

e) Kamati ya usimamizi wa miradi itatoa taarifa ya uendeshaji wa mradi kwa Kamati/Bodi ya Shule.

f) Kumbukumbu za maendeleo ya utekelezaji wa mradi ikiwemo mapato na matumizi zitunzwe kwenye jalada la taarifa za mradi na pia ziwekwe wazi kupitia mbao za matangazo na kwenye vikao vya shule.

g) Wanafunzi washirikishwe kwenye shughuli stahiki za utekelezaji wa mradi ambazo hazitaathiri ratiba ya vipindi vya darasani kama vile kumwagilia bustani, kulisha kuku, na kuhudumia mifugo ili kupata ujuzi wanapofanya kazi kwa vitendo ndipo wanavyoelewa.

## 6.0 Majukumu ya Wadau Mbalimbali

### 6.1 Kamati/Bodi ya Shule

i) Kuandaa, Kusimamia, na Kuhakikisha mradi wa Shuleunatekelezwa kwa ufanisi;

ii) Kuhakikisha kuwa mapato yanayopatikana katika mradi wa shule yanawekwa wazi na kutumika kwa utaratibu uliokubaliwa.

iii) Kuhakikisha taarifa za mapato na matumizi ya miradi ya shule zinatunzwa na zinatolewa kupitia vikao mbalimbali na kuwekwa wazi kwenye mbao za matangazo za shule.

### 6.2 Mwalimu Mkuu/Mkuu wa Shule

i) Kusimamia uanzishwaji na utekelezaji wa miradi ya shule kwa kusaidiwa na timu ya menejimenti ya shule na kamati ya uzalishaji mali ya shule;

ii) Kuratibu mapato, matumizi na uwekezaji katika mradi;

iii) Kuteua wajumbe wa kamati ya Elimu ya Kujitegemea;

iv) Kupanga ratiba ya vipindi vya uzalishaji mali, ratiba hiyo ibainishwe katika Kalenda ya utekelezaji wa shughuli za shule nje ya darasa;

v) Kushirikiana na kamati ya elimu ya kujitegemea kuandaa taarifa ya uzalishaji mali na kuiwasilisha kwenye kamati/ bodi ya shule;

vi) Kutunza kumbukumbu za miradi ya shule;

vii) Kutoa taarifa za maendeleo ya miradi kwa wadau wote wa shule ambao ni Kamati/bodi ya shule, walimu, wanafunzi, Afisa elimu Kata na uongozi wa Halmashauri husika; na

viii) Kuhakikisha kuwa jamii inashirikishwa katika kubuni na kutekeleza miradi ya shule.

## 6.3 Kamati ya Elimu ya Kujitegemea

Muundo wa kamati ya uzalishaji mali ya shule utazingatia maelekezo yaliyopo kwenye Kiongozi cha Mkuu wa Shule Tanzania Bara. Shughuli zake zitakuwa kama zilivyoelekezwa katika kiongozi hicho ambazo ni pamoja na;

i) Kusimamia miradi ya uzalishaji mali; na

ii) Kutunza kumbukumbu na kutoa taarifa kwa Mkuu wa Shule na Kikao cha Walimu.

### 6.3.1 Wajumbe wa Kamati

Wajumbe wa kamati ni kama ifuatavyo:

i) Mwenyekiti: atakuwa Mkuu wa shule/Mwalimu Mkuu ;

ii) Katibu: atachaguliwa na wajumbe wa kamati;

iii) Mratibu wa Miradi: atateuliwa na Mkuu wa Shule/Mwalimu Mkuu;

iv) Mhasibu wa Shule;

v) Ofisa Manunuzi wa Shule;

vi) Mwalimu wa nidhamu wa Shule ;

vii) Mwalimu Mlezi wa Mradi; na

viii) Kiongozi wa Elimu ya Kujitegemea wa Wanafunzi.

Mkuu wa Shule/Mwalimu Mkuu anaweza kuongeza wajumbe wengine kulingana na mahitaji au mazingira ya shule husika.

### 6.3.2 Majukumu ya Kamati ya Elimu ya Kujitegemea

i) Kushiriki katika kubuni, kuanzisha na kusimamia miradi ya uzalishaji mali shuleni;

ii) Kuandaa andiko la mradi;

iii) Kuweka mipango ya utekelezaji wa kazi za uzalishaji mali ;

iv) Kutunza kumbukumbu na kutoa taarifa ya uendeshaji wa miradi kwa Mkuu wa Shule/Mwalimu Mkuu;

v) Kupokea taarifa za kila mradi kutoka kwa Mwalimu Mlezi wa Mradi;

vi) Kutoa ushauri kwa Mkuu wa Shule kuhusu ufanisi wa miradi ndani ya shule;

vii) Kutayarisha makadirio ya mapato na matumizi ya miradi ya shule; na

viii) Kusimamia utekelezaji wa shughuli mbalimbali za kuhudumia miradi ya uzalishai mali shuleni.

**6.4 Afisa Elimu Kata, Halmashauri na Mkoa**

Maafisa Elimu wa Kata, Halmashauri na Mkoa watahakikisha kuwa shule zao zote zinatoa Elimu ya Kujitegemea kwa vitendo kwa kuanzisha miradi ya uzalishaji mali na kuhakikisha kuwa miradi inasimamiwa kwa ufanisi na kuwa na tija.

**6.5 Maofisa Maendeleo ya Jamii**

Maafisa maendeleo ya jamii watafanya kazi ya kukagua na kufanya ufuatiliaji wa miradi inayoendeshwa shuleni na kutoa ushauri unapohitajika

**6.6 Mratibu wa Elimu ya Kujitegemea Kila Shule itakuwa na mratibu wa elimu ya kujitegemea (MEK) atafanya kazi chini ya kamati ya uzalishaji mali ya shule. Majukumu yake yatakuwa:**

i) Kuratibu miradi yote ya uzalishaji mali shuleni;

ii) Kuwa katibu wa kamati ya uzalishaji mali, pia ataandaa na kuandika taarifa mbalimbali za uzalishaji mali;

iii) Kuratibu makusanyo ya maduhuli yatokanayo na miradi ya shule;

iv) Kutunza mali na vifaa vya Miradi ya shule;

v) Kubuni miradi mipya shuleni; na

vi) Kutunza kumbukumbu za mapato na matumizi ya miradi yote shule.

**6.7 Kiongozi wa Wanafunzi wa Elimu ya Kujitegemea**

Miradi inayoanzishwa Shuleni iwe na kiongozi wa Wanafunzi anayesimamia Elimu ya Kujitegemea. Kiongozi wa mradi atakuwa na wajibu na madaraka yafuatayo:

i) Kushiriki katika vikao vya kamati ya Elimu ya Kujitegemea;

ii) Kusimamia wanafunzi katika kutekeleza shughuli mbalimbali za uzalishaji mali; na

iii) Kuhakikiisha wanafunzi wanapata taarifa za mapato na matumizi ya fedha za miradi ya shule.

## 6.8 Mhasibu wa Shule

Mhasibu wa shule atashiriki kutunza hesabu zinazohusu uendeshaji wa miradi shuleni. Jukumu hilo litahusisha:

i) Kutayarisha na kutoa malipo yanayohusu miradi ya shule kwa kuzingatia Sheria na taratibu zilizopo;

ii) Kupokea na kuhifadhi fedha za miradi; na

iii) Kutayarisha, kutawanya na kutunza kumbukumbu za hesabu za miradi ya shule. Hesabu zitakazosajiliwa na mhasibu/ msarifu ni kama ifuatavyo:

  a) Hesabu katika leja: Kwenye leja mhasibu ataingiza hesabu ya kila mradi na Takwimu zitapatikana kutoka kwa mwenyekiti wa miradi;

  a) Daftari la Fedha: Kila mara mhasibu/msarifu anapopokea fedha kutoka kwa kiongozi wa Elimu ya Kujitegemea, atatoa stakabadhi ya fedha na ataingiza mapokeo hayo kwenye leja ya mradi unaohusika. Namba za hati za malipo zitolewazo kwa kiongozi wa mradi ili aweze kuziingiza katika hesabu yake ya fedha. Pia ataonesha urari, faida, hasara na mizania ya miradi yote.

## 7.0 Matumizi ya Mapato yanayotokana na Miradi ya Kuzalisha Mali

Mapato yanayotokana na miradi ya uzalishaji mali shuleni yanaweza kutumika katika shughuli mbalimbali za uendeshaji wa shule kama vile chakula na Motisha kwa Wanafunzi na Wafanyakazi.

## 8.0 Uuzaji wa Mazao au Vifaa/Bidhaa

Kila shule inaagizwa iwe na mipango mizuri ya kutafuta soko la kuuzia mali inayozalishwa shuleni. Shule inaweza kuuza mazao yanayotokana na miradi yake kwa kufuata taratibu.

## 9.0 Motisha kwa Wanafunzi na Wafanyakazi

Ili kudumisha ari ya wanafunzi na wafanyakazi katika kushiriki kikamilifu katika kazi za kuzalisha mali, shule inashauriwa kuzingatia mambo yafuatayo:

i) Wafanyakazi na wanafunzi wapewe taarifa za uzalishaji mali kila baada ya miezi mitatu;

ii) Wafanyakazi na wanafunzi wapewe nafasi ya kujadili na kutoa mawazo kuhusu mipango ya uzalishaji mali na uendeshaji wake;

iii) Wafanyakazi wa shule wanaweza kuruhusiwa kununua mazao/vifaa vinavyotokana na miradi ya shuleni. Bei zitaamuliwa na vikao vilivyotajwa katika mwongozo huu; na

iv) Juhudi ya kila mwanafunzi na wafanyakazi katika kuzalisha mali ipimwe; na wale wanaojitokeza wapewe tuzo.

## 10.0 Ukaguzi wa Fedha za Miradi ya Sshule

Ukaguzi wa fedha za miradi ya shule utafanywa kwa kuzingatia sheria na taratibu za ukaguzi wa fedha za Serikali.

## 11.0 Taarifa ya Uzalishaji Mali

Kila shule itatakiwa kuandaa na kuwasilisha taarifa ya maendeleo ya uzalishaji mali kwa kamati/Bodi ya Shule, walimu, wafanyakazi wasio walimu na wanafunzi kupitia vikao rasmi. Pia, kuhakikiska tarifa za mapato na matumizi zitakuwa wazi katika mbao za matangazo.

## 12.0 Hitimisho

Elimu ya Kujitegemea huchangia katika kupata ujuzi, maarifa, stadi za kazi na mwelekeo chanya wa maendeleo ya wanafunzi na Taifa kwa ujumla. Hivyo Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inatarajia kuona kwamba shule za msingi na sekondari zinaanzisha na kusimamia miradi mbalimbali ya uzalishaji mali kwa kuwashirikisha wanafunzi na wataalamu kutoka katika taasisi mbalimbali. Miradi inayoweza kuanzishwa ni pamoja na ufugaji wa wanyama, kilimo cha mazao ya mbogamboga, mashine za kusaga na kukoboa, mashine za kutotolea vifaranga vya kuku, na ufugaji wa samaki. Uanzishwaji wa miradi hiyo itawawezesha wanafunzi kujifunza kwa vitendo shughuli mbalimbali za uzalishaji mali na kuziwezesha shule kujipatia kipato kitakachochangia katika uendeshaji wake.

# Rejea


Bundy, D., Burbano, C., Grosh, M., Gelli, A., Jukes, M. And Drake, L. *(2009). Rethinking school feeding:* Social safety nets, child development, and the education sector. Washington DC: World Bank.

Nyerere, J, K. (1967). *Elimu ya kujitegemea*. Mpigachapa Mkuu wa Serikali. Dar es Salaam.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (2013). *Kiongozi cha mwalimu mkuu, uboreshaji wa elimu katika shule za msingi*, Dar es Salaam.

Wizara ya Elimu ya Taifa. (1982). *Kitabu cha uongozi katika vyuo vya ualimu.* Printpak/ MTUU. Dar es Salaam.

WyEST. (2014). *Sera ya elimu na mafunzo*. Dar es salaam

WyFM. (2016). *Mpango wa maendeleo wa taifa wa miaka mitano 2016/17-2020/21.* Dar es Salaam.